ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa na Rais
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
43.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
44.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
45.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
47.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
48.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
49.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake

50.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Jimbo la Kikwajuni

51.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk Jimbo la Kitope

52.Mhe. Marina Joel Thomas Kateuliwa na Rais

53.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

54.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

55.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

56.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

57.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

58.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

59.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

61. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

66.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

69.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

70.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

71.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

76.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 24 Oktoba, 2012

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 67

Utengenezaji wa Barabara za Ndani

Mhe. Suleiman Hemed Khamis – Aliuliza:-

Tunapotembelea miji ya Unguja na Pemba tunaona jinsi gani miji hiyo barabara zake za ndani yaani (*feeder roads*) zilivyoathirika kwa mashimo makubwa kama vile Wizara haipo au imepata likizo, mfano njia ya Mkunazini, mji wa Chake-Chake na eneo la kupinda kuingia ndani kabla ya (*parking*) Darajani.

Je, ni lini barabara hizo zitafanyiwa matengenezo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ninamshukuru Allah kwa kutupa uhai na uzima, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Suleiman Hemed Khamis wa Jimbo la Konde kama hivi ifuatavyo:-

Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara (UUB) imepewa majukumu ya kujenga na kutunza mtandao wa barabara kuu (*Trunk Roads*), barabara za vijijini (*Rural roads*) na barabara zinazounganisha ama barabara kuu au barabara za vijijini yaani (*feeder roads*). Barabara hizo zimeorodheshwa kwenye sheria ya barabara sura ya 134 (Cap 134), barabara alizozitaja Mhe. Suleiman Hemed Khamis kwa mujibu wa sheria zilizopo zipo kwenye Mamlaka ya Wizara ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ kwa maana ya Manispaa, na barabara za mji wa Zanzibar na halmashauri za Wilaya hizo kutotenga bajeti na ukosefu wa wataalamu wa kuzifanyia matengenezo barabara za mji wa Zanzibar na halmashauri za miji au Wilaya kwa maeneo mengine.

Hata hivyo, kutokana na Manispaa na Halmashauri za Wilaya hizo kutotenga bajeti na ukosefu wa wataalamu wa kuzifanyia matengenezo barabara zao, kazi za matengenezo/ujenzi wa barabara hizo zimekuwa zikifanywa na Wizara yangu kwa kushirikiana na mfuko wa barabara, na hivyo kuzoeleka kuwa barabara zote ziko chini ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza awali, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mfuko wa barabara imeanza kuzifanyia matengenezo barabara ya Mkunazini na zile za mji wa Chake Chake ikiwa pamoja na kuziba mashimo sehemu ya kuingia daladala hapo Darajani. Hata hivyo, namthibitishia Mheshimiwa kuwa Wizara yangu ipo, haijalala na kwamwe haitolala, kazi za utunzaji wa barabara zinaonekana na nachukua nafasi hii kuwaelezea wananchi watoe mashirikiano yao ya kuzitunza barabara zao na wasiziharibu kwa makusudi kwa kuzichoma moto.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa sasa hivi kuna manung'uniko makubwa kwa njia za ndani, ambazo njia hizi za ndani zina vibali ya gari ambayo vinapita katika maeneo yale ambao barabara hizi ni mbovu zilizoungana na barabara kuu. Ni lini hasa Wizara yake itashughulikia barabara hizi za *feeder roads*.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa kuwa *feeder roads* ziko nyingi, Wizara ina utaratibu kupitia UUB kuchagua kwa kila Wilaya idadi fulani kutokana na bajeti iliyopo, na kwa hivyo kuna

maendeleo ya kila Wilaya kwa kila bajeti kwamba njia fulani zitatengenezwa. Na utaratibu huu upo kimaandishi na kama anataka tunaweza kumletea kimaandishi kwa bajeti ya mwaka huu 2012/2013 ni barabara gani za *feeder roads* ambazo zimetengewa kupitia mfuko wa barabara ili ziweze kutengenezwa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi asubuhi hii kuweza kumuuliza swali la nyongeza Mheshimiwa Waziri ambaye alikuwa Makamo Mwenyekiti wangu. Mheshimiwa katika awamu ya mwanzo ulisema kuwa barabara za *feeder roads* kama ikiwa mashamba ni wenyewe halmashauri, ikiwa mjini ni wenyewe Manispaa. Lakini sasa hivi umesema kuwa ndani ya watu wa barabara wana uwezo wa kutengeneza barabara hizi. Je, Mheshimiwa hebu nipe jibu sahihi kati ya hao nani wenye sheria ya kuziendeleza hizo *feeder roads*.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, katika majibu ya awali nilisema kwamba *feeder roads* ni sehemu ya UUB isipokuwa barabara zinazopita katika sehemu za miji kwa Manispaa ya Zanzibar na sehemu za miji ya Chake Chake Wete na Mkoani, kwa mabaraza ya miji ya Chake Chake, Mkoani na Wete. Hizi ziko chini ya mamlaka ya zile Manispaa au Mabaraza ya Miji.

Lakini kutokana na ukosefu wa kiutaalamu na Mipango kamilifu, ambayo jana Mhe. Spika, ilishuhudia hapa Baraza likipokea ripoti rasmi kuhusu utendaji wa Manispaa. Sasa kutokana na udhaifu ule uliopo ndio mfuko wa barabara hushirikiana na UUB zinatengeneza hizi barabara za miji ambazo tayari zilikuwa ziko moja kwa moja kwenye Manispaa au Halmashauri za miji.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa na mimi naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwanza niipongeze Wizara ya Miundombinu kwa jitihada ambazo zimeanza kuonekana katika kubadilisha mazingira ya ujenzi wa barabara na hususan za *feeder roads* katika maeneo mbali mbali. Miongoni waliofaidika na mimi ni mmoja kupitia mfuko wa barabara ya Mikunguni/Muembenjugu na kwa Jumapweza/Kwaalamsha. Lakini swali langu lipo hapa Mhe. Spika, kabla ya barabara hizo kufanyiwa marekebisho barabara zetu hizo za ndani zilikuwa zimewekwa matuta ili kuondosha kadhia za ajali za mara kwa mara. Lakini bado matuta ya maeneo hayo hadi leo hayajarejeshwa na kipindi kimekuwa kirefu na tayari ajali na vifo vimeshaanza kutokea.

Je, Mhe. Waziri ananipa tamko gani katika hili.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa kuwa utaratibu wa kuweka matuta ni utaratibu wa kiutaalamu, kwa hivyo mimi ninalipokea swali hilo na nategemea kwamba iwapo utaalamu unaruhusu maeneo hayo kuwekwa matuta basi bila ya wasiwasi yatawekwa kulinda usalama. Lakini kuna utaratibu wa kuweka na alama za zebra ambayo vile vile ni sehemu moja ya kulinda usalama wa raia.

Nam. 71

Tatizo katika Usambazaji Umeme

Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Aliuliza:

Shirika la Umeme huingia mkataba na wananchi katika usambazaji na utiaji umeme katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu. Muda unaotolewa kwa shughuli za kazi hiyo ni mzuri na unajenga matumaini kwa kazi ya usambazaji wa nguzo, uwekaji wa nyaya na uingizaji wa umeme ndani ya nyumba ni ahadi anazopewa mwananchi. Lakini matokeo yake yanakatisha tamaa kwa wananchi kwani mwaka utafika bila ya mafanikio.

Mhe. Waziri ahadi wanazotoa wanaohusika ni ahadi zinazotekelezwa kwa wakati wanaokubaliana. Je, hatua gani utachukua kuhakikisha kwamba ahadi hizo ziwe za kweli zisizo na usumbufu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 71 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ahadi zinazotolewa na Shirika la Umeme ni za kweli na wala si za kuwasumbua wananchi. Ni mara chache ahadi hizo kuchelewa kutokana na ukosefu ama kuchelewa kwa vifaa, ambavyo husababishwa na uagiziaji vifaa kwa mfumo wa kizamani kwa njia ya "Analog" – lakini kwa sasa Shirika limenza kujipanga katika uagiziaji wa vifaa hivyo kwa njia ya "Digital" jambo ambalo litasababisha kufika vifaa, hivyo haraka na kuwaondoshea wananchi usumbufu huo na kuwapelekea huduma hiyo kwa wakati muafaka kama tulivyoahidi.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Waziri je, kuna ahadi ngapi kwa Unguja na Pemba ambazo bado hazijatekelezwa. Na ikiwa hazijatekelezwa kwa nini.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, ahadi zilizokuwepo Unguja na Pemba ni nyingi, na kilichosababishwa kutotekelezwa kama nilivyoeleza huko nyuma hapo awali kwamba kutokana na uchelewaji wa vifaa hivyo ni kitu ambacho kinasababisha kuchelewa kutekelezwa ahadi hizo. Lakini nimuahidi Mhe. Mwakilishi kwa mfumo ambao tunaenda nao sasa hivi wa uagiziaji wa vifaa hivyo, basi ninamuhakikishia kwamba ahadi zote tutazitekeleza na kwa wakati muafaka.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa moja katika vifaa muhimu sana vya umeme ni mita, na utaratibu ambao Shirika walikuwa nao kwa yule ambaye mita yake imeharibika, basi walikuwa wanambadilishia mita ya Tukuza kutoka ile ya ringi. Na kazi hiyo walikuwa wakiifanya bure wanaondoa ile wanatia ile. Lakini utaratibu wa sasa hivi imekuja tu wananchi wanalipishwa pesa nyingi kama kwamba wamekwenda kuomba wauziwe mita ya Tukuza. Naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri ilikuwaje hata huu utaratibu ukabadilika kutoka kubadilishiwa bure na sasa wanauziwa kwa shilingi karibu laki moja na arobaini.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, utaratibu wetu wa Shirika la Umeme inapoungua mita ya mteja wetu yoyote basi tunambadilishia mita hiyo bila ya malipo yoyote. Na kama limefanyika suala hilo kwa mfanyakazi wetu basi ningeomba Mhe. Mwakilishi tulifuatilie pamoja suala hilo ili tulipatie ufumbuzi. Lakini mita yoyote ikiwa ya Tukuza au ikiwa mita ya kawaida basi inapoharibika kwa mteja wetu basi tunafunga mita hiyo bila ya kumlipisha faini au kumtoza pesa yoyote kwa ajili ya kufungiwa mita hiyo.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ahadi ni deni na kwa kuwa suala la umeme kijiji cha Muuka uliniahidi kwamba utalifuatilia tukiwa mimi na wewe pamoja. Hadi hii leo Mhe. Waziri sijapata salamu zako wala ahadi zako ulizoziweka. Je, Mhe. Naibu Waziri kutolifuatilia suala hili kwa wananchi wa Muuka je, huoni ni kuwanyima haki zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kama nilivyomuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba niko tayari kulifuatilia tatizo hilo pamoja na yeye ili nipate wepesi wa kwenda kulijua hilo tatizo basi lazima niwe pamoja na yeye. Na yeye nakumbuka nimemjibu nikamwambia nimempa nafasi ya upendeleo, kwa hivyo mimi nipo tayari wakati wowote atakapokuwa tayari yeye anipe taarifa na tutalifuatilia kwa pamoja wakati wowote saa yoyote.

Nam. 15

Utaratibu wa Kumaliza Mabanda

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Sera ya Wizara ya Elimu ni kumalizia mabanda yote ya skuli yaliyofikia hatua ya kuezeka. Kwa kuwa kuna maeneo mengi yenye mabanda yaliyofikia hatua hiyo.

Je, Wizara ina utaratibu (*formula*) maalum wa kumalizia majengo hayo ili kuepusha upendeleo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe.Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma Mwakilishi wa Jimbo la Wawi swali lake namba 15 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika**,** Ni kweli kuwa ni Sera ya Serikali kumaliza majengo ya Skuli yanayojengwa na wananchi yanapofikia sehemu linta ili majengo yale yaweze kutumika. Ni kweli kwamba yapo majengo mengi ambayo yamejengwa yamemalizika yamefika kiwango hicho hicho na bado hatujayamaliza. Hili linatokana na uhaba wa bajeti yetu tunayopata kila mwaka.

Lakini ameuliza kwamba je nimeandaa mpango gani sasa kuyamaliza majengo hayo bila ya upendeleo. Nataka nimuhakikishie kwamba kadiri ya bajeti yangu itakavyoniruhusu na mwaka huu nataka nimuahidi Mheshimiwa Mwakilishi kwamba bajeti yangu safari hii ni nzuri kidogo na nimeshajipanga nimeshajitayarisha, na nimeshazichagua baadhi ya skuli ambazo zinaweza kukamilishwa kwa bajeti hiyo.

Na kigezo nitakachokitumia kuzikamilisha skuli hizo ni kwanza lini wananchi walimaliza kuzijenga skuli hizo. Pili, ziko katika eneo gani ambalo lina uhaba wa majengo na lina wanafunzi wengi. Tatu, fedha zilizopo zinaweza kutosheleza kuimaliza kazi hiyo ambayo nitakayoianza.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana aliyoyatoa Mhe. Waziri, na kwa kuwa Mhe. Waziri amesema kuwa tayari wameshajipanga ninashukuru leo hajatumia kama wapo mbioni lakini kujipanga ni upande mmoja na utekelezaji ni upande wa Pili. Je Mhe. Spika, Mhe. Waziri ana habari kwamba skuli ya Ng'ambwa katika Jimbo la Wawi na skuli ya Vitongoji kuna mabanda karibu mwaka wa kumi yamemalizika na hili la ng'ambwa liko katika ahadi ya Rais Mstaafu Mhe. Amaan Abeid Amaan Karume kwamba lingeezekwa haraka iwezekanavyo tangu mwaka 1998 unayo habari hiyo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kuhusiana na skuli ya Mwambe napenda kumuahidi katika Baraza hili mara tu fedha zitakapoingia tutaanza kuikamilisha hiyo kazi tuliyoiahidi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ninakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa na mimi nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri aliyoyaeleza Mhe. Waziri na ninashukuru sana Mhe. Waziri kasema bajeti yake zamu hii inamruhusu na imekuwa zaidi. Kwa hivyo *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu katuahidi kama atatekeleza mara tu bajeti yake itakapomruhusu. Lakini je, ninamuuliza Mhe.Waziri kwa kuwa skuli ya Micheweni kuna mabanda yaliyojengwa zamani ambayo ndio yaliyoanza kusomewa na mabanda hayo kuna moja tayari limeshaharibika mapaa yake na dari yake na sasa hivi linaanza kuporomoka ni hatari hata kwa watoto ambao kuwa wanasoma. Je katika bajeti hiyo na banda hilo ataliangalia. Na kama ataliangalia ananipa ahadi gani ili wananchi wamsikie.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nilipokuwa nikitoa majibu mama nilisema kuzimaliza skuli hizi zilizojengwa na wananchi kufikia katika hicho kiwango tulichokiahidi, na naomba hata kabla sijaliendeleza swali hili nataka nitoe kauli ya kuwashukuru sana wananchi kwa kuitikia wito huu wa kuzijenga skuli zetu ili kuwapatia watoto wetu sote nafasi za kusoma katika madarasa yaliyojengwa.

Sasa nikiendelea kulijibu hili swali nasema nilitoa vigezo vya skuli baada ya skuli kuziendeleza na kuzimaliza. Ni kweli nimesema bajeti ya mwaka huu ni nzuri kidogo ni kweli kabisa ni nzuri na nimesema tumeshajipanga kuziendeleza skuli hizi kwa utaratibu nilioutaja ikiwemo pahala ilipo hapo skuli penye watoto wengi mahitaji makubwa na watoto hawana pa kukaa.

Sasa kama Skuli ya Micheweni nayo itaingia katika utaratibu huo wa mipango hiyo niliyoipanga kama ilivyoingia Skuli ya Mwambe nasema na hiyo pia tutaiangalia na ikiwezekana mwaka huu tutaitengeneza. Lakini nataka nimwambie Mheshimiwa Mwakilishi kwamba katika eneo la Micheweni kuna mabanda mengi sana yameshakamilika na yameshatengenezwa ni mazuri na wanafunzi wanakaa wanasomea, wanayatumia. Nasema tena kama itaonekana haja hiyo ipo kwamba wanafunzi waliopo Micheweni ni wengi hawana pa kukaa nitachukua hatua hiyo.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri katika vigezo ulivyotajwa amesema kwamba atatizama skuli ambayo imejengwa kwa muda

mrefu, yenye mahitaji makubwa kwa wanafunzi lakini yangu ina sifa ya ziada. Iko kijijini Mwachealale na ya muda mrefu na mwaka huu kama haikumalizwa itabidi watoto wahamishwe Mwachealale warudi Mfenesini, ni tatizo kidogo je na hii ataipa kipaumbele.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nilijua Mhe. Ali Abdalla ataniuliza swali hili kwa sababu ni kweli kabisa yeye ni miongoni mwa Wawakilishi waliomaliza skuli zao na zimekaa muda mrefu. Hilo halina pingamizi zinaingia katika yale maeneo niliyosema nikiyagundua kuna maeneo hayo mahitaji makubwa, skuli zimejengwa muda mrefu nitachukua hatua za kuzikamilisha.

Nam. 16

Chuo cha *SUZA* Kutoanzisha baadhi ya Fani

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Katika kukabiliana na mabadiliko ya Tabia Nchi, sambamba na kuengeza kipato kwa wakulima, Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) tangu zamani hadi sasa kimeazimia kuanzisha Digirii ya mwanzo ya Mazingira, sambamba na kufungua Kitengo cha Kilimo Tawi la Pemba *(Faculty of Agriculture Pemba Branch).*

Je, ni sababu gani za msingi zilizosababisha hadi leo hii azma hiyo isitekelezwe.

Mhe.Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa mkereketwa wangu Saleh Nassor Juma swali lake Namba 16 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Wawi aliyechaguliwa kwa kura nyingi sana kwamba ni kweli tunayo sera hiyo na tunayo azma ya kuitekeleza sera hiyo ya kuanzisha somo la Digirii ya kwanza la Mazingira au Hifadhi ya kutokana na mabadiliko makubwa sana ya Tabia Nchi. Nataka nimuhakikishie mwaka ujao 2013 tutaanzisha somo hilo la Digirii ya Kwanza ya Mazingira.

Mipango ya kutayarisha *syllabus*, mipango ya kutafuta walimu inakaribia kukamilika na itakamilika kabla ya kufika mwaka huona na kufika wakati huo tuliokusudia kuteleza hilo agizo au sera ya Wizara au Elimu Chuo cha *SUZA*.

Napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba Chuo hicho kitaanzisha somo hilo mwakani kama tulivyoahidi mwaka 2013.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana yanayotia moyo na yanayoashiria maendeleo ya nchi yetu aliyonijibu Mhe. Waziri naomba niulize swali dogo sana la nyongeza. Pamoja na kuanzisha *faculty of environment* katika SUZA nilizungumzia kwamba walikuwa vile vile na lengo la kuanzisha *Faculty of Agriculture.* Nadhani waziri kwa kuwa hivi sasa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzíbar yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa katika kukabiliana na umasikini na kuongeza kipato kwa wananchi wetu imeamua kuleta Mapinduzi ya Kilimo. Je, haoni hii dhamira ya kufungua *faculty of agriculture* ingesaidia sana serikali hii kuboresha kilimo pamoja na kuleta maendeleo katika nchi yetu, lakini kwa nini hakunijibu kama wataanzisha au hawataanzisha.

Mhe.Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, Chuo Kikuu cha *SUZA* kina hamu kubwa sana ya kuanzisha *faculties* mbali mbali zikiwemo hiyo ya kilimo na kadhalika. Inategemea sasa uwezo wa kifedha, inategemea uwezo wa wasomeshaji na kadhalika, ndio maana tumechagua kwenda *faculty* kwa *faculty* hadi tufikie kuzisomesha hizo *faculty* zilizokuwa muhimu zitakazowasaidia wananchi kiuchumi kama hii *faculty* ya *agriculture* aliyoizungumza Mheshimiwa.

Namuomba Mhe. Mjumbe tuvute subira kidogo tumalize hii *faculty* ya mazingira tuianzishe na ikitulia huku tunaendelea kuazisha *faculty* nyengine za kilimo, uvuvi na kadhalika. Kwa hivyo, naheshimu sana swali lake la nyongeza na ni swali zuri na Chuo Kikuu cha *SUZA* kimejitayarisha kufanya hivyo lakini sote tunajua kuanzisha *faculty* ya Chuo Kikuu si kazi ndogo, si kazi rahisi inahitaji wataalamu, walimu na inahitaji fedha. Kwa hivyo, natumai Mhe. Mjumbe atanikubalia kwamba tutakwenda *faculty* kwa *faculty* pole pole na hatimaye tutakamilisha.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza lenye vifungu a na b.

(a) Mhe. Spika, mara kadhaa Chuo cha *SUZA* kimekuwa kikilalamika kwa kukosa maabara inayolingana na hadhi ya chuo kulingana na uchache wa fedha. Sasa tuliwahi kuambiwa kwamba wanahitaji si chini ya shilingi milioni 200 ili kuiboresha maabara ya *SUZA* ilingane na vyuo vyengine hapa Tanzania. Sasa naomba kujua gharama ambayo itaigharimu *SUZA* kwa kuanzisha *degree* ya kwanza ya mazingira na ile gharama ambayo ingegharimu *SUZA* kwa kuboresha maabara ya *SUZA* ni ipi itakuwa gharama kubwa.

(b) Serikali iliwahi kutwambia mara kadhaa kwamba iliunda kamati kwa ajili ya kuangalia uwezekano wa kuunganisha Chuo cha Afya Mbweni na Chuo cha Kilimo Kizimbani iwe sehemu ya *SUZA* kusudi kwamba ile *degree* au *faculty* ya *agriculture* iweze kuendelezwa. Kwa nini *SUZA* wanaamua kuanzisha *degree* ya mazingira na kwanza tusipewe ile taarifa ya tume ambayo ilipendekeza *faculty* ya *agriculture* kuitoa Kizimbani ianze mwanzo kama sehemu ya *SUZA*.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nakubaliana na yeye moja kwa moja kwamba ni kweli kuanzisha maabara ni fedha nyingi, sina hakika hizo alizozitaja ni sahihi nataka nizifuatilie nipate na mimi kujua kwamba ni kweli pesa hizo ni sahihi na ndizo zinazohitajika kuanzisha maabara hiyo.

Katika jengo jipya tulilolijenga kule Tunguu ambalo linakaribia sana kumalizika na kuna tamaa kubwa sana tutalihamia hivi karibuni, maabara, majengo ya *practicals* na kadhalika yamejengwa yapo na kuna *faculty* moja ya *engineering* majengo yake pia yameshakamilika yapo. Kwa hivyo, bado nataka niseme umasikini bado umetuzonga, kuchagua hili ukaacha hili ni kazi kubwa na ni kazi ngumu, lakini tuko mbioni kutafuta kila mbinu za kupata hizo fedha kama ni misaada, kama ni mikopo ya Benki Kuu za Dunia za ulimwenguni, lakini hatimaye kama tulivyofikia hivi sasa tutafikia pazuri zaidi, tutakamilisha maabara tutajenga na hayo manung'uniko yataondoka, tumuombe Mwenyezi Mungu atusaidie.

La pili naomba Mheshmiwa alirejee swali lake la (b).

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, swali la pili ni kwamba, serikali iliwahi kutwambia mara kadhaa kwamba iliunda kamati kwa ajili ya kuangalia uwezekano wa kuunganisha Chuo cha Afya Mbweni na Chuo cha Kilimo Kizimbani iwe sehemu ya *SUZA* kusudi kwamba ile *degree* au *faculty* ya *agriculture* iweze kuendelezwa. Kwa nini wasianze ile ripoti ya tume kwanza na badala yake wanaanza kuandaa *degree* nyengine mpya ya mazingira wakati ile ripoti ya tume ipo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli serikali imeunda tume na tume hii inakaribia kukamilisha kazi zake na kuwasilisha taarifa yake. Mhe. Spika, kuna usemi wa kiongozi wetu mmoja mkubwa anayesema kupanga ni kuchagua. Taarifa ya tume na haja ya kujenga au ya kuanzisha elimu ya tabia nchi ni kupanga na kuchagua. Mhe. Spika, mabadiliko ya tabia nchi sasa hivi ni makubwa sana, yanatuathiri sana, yanaathiri hata miongo yetu ya kuishi kwetu, hatujui mvua ya masika itaanza lini na itamalizika lini, hatujui kilimo cha mpunga kinaanza lini kitamalizika lini. Kwa hivyo, bado kupanga ni kuchagua tutayaangalia yote mawili ya tume na ya maombi ya Baraza hili kukumbushwa Baraza hili ya kuanzisha *faculty* ya tabia nchi (ya mazingira) hatimaye tutaleta taarifa kwenye Baraza hili pale ambapo tutaamua pa kuanzia. Ahsante sana.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Baharini Nam. 5 ya Mwaka 2006

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usafiri Baharini Nam. 5 ya Mwaka 2006 kusomwa mara ya mwanzo.

Mhe. Spika: Sasa mimi nadhani usome huo mswada wenyewe halafu tena utakuwa unawasilisha rasmi.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usafiri Baharini Nam. 5 ya Mwaka 2006 kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika: Hivi jina refu la mswada likoje?

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Baharini Nam.5 ya mwaka 2006 na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika: Ahsante sana mswada huo umeshasomwa kwa mara ya kwanza hii maana yake ni kwamba, mswada huo tayari uje kufanyiwa kazi na kamati inayohusika. Tuendelee.

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Utangazaji Zanzíbar,
Kazi, Majukumu na Utawala wake

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Utangazaji Zanzíbar, Kazi, Majukumu na Utawala wake pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika: Ahsante sana anaomba mswada huo usomwe kwa mara ya kwanza na kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe naomba pia mpokee mswada huo wa kusomwa kwa mara ya kwanza kwa maana ya kwamba kamati inayohusika uufanyie kazi baadae kwa matayarisho ya kuja kusomwa kwa mara ya Pili.

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Meli Zanzíbar

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Meli Zanzibar, Kazi, Uwezo na mambo mengine yanayohusiana na hayo kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri mswada umesomwa kwa mara ya kwanza kamati inayohusika itaufanyia kazi ili kujitayarisha na shughuli hiyo kwa kusomwa mara ya Pili Baraza lijalo.

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya
Ruzuku kwa Vyama vya Siasa Nam. 6 ya 1957

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa Nam. 6 ya mwaka 1957 na mambo yanayohusiana nayo kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika: Mswada umesomwa kwa mara ya kwanza nao pia kamati inayohusika wataufanyia kazi kwa matayarisho ya kusomwa kwa mara ya Pili.

Waheshimiwa Wajumbe ili tumkaribishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atoe hotuba ya kufunga mkutano huu naomba nitangulie kuchukua nafasi hii kwanza kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya, kujibu maswali, kupitisha miswada pamoja na Ripoti ya Serikali na Ripoti ya Kamati Teule. Kazi hiyo Waheshimiwa Wajumbe mmeifanya kwa ufanisi mkubwa nichukue nafasi hii kuwapongeza sana kwa kazi hiyo nzuri, lakini kazi hiyo nzuri isingeweza kufikia hapo kwa kiwango hicho kama si kwa kazi ya matayarisho makubwa yaliyofanywa na Makatibu wakiongozwa na Katibu wa Baraza la Wawakilishi ambao nao kwa mashirikiano wametayarisha mkutano huu mzima hadi kufikia leo tunamaliza shughuli zetu.

Waandishi wa Habari, Watafsiri wetu pale, wametusaidia sana kutoa taarifa hizo kwa umma juu ya shughuli inayoendelea hapa. Napenda kuchukua nafasi hii kuwaomba sana Waheshimiwa Wajumbe tuendelee kushirikiana kwa karibu sana katika utekelezaji wa shughuli zetu bila ya kuwa na migongano yoyote. Hii itasaidia kutimiza wajibu wetu wa kikatiba kuendesha shughuli zetu kama inavyoelekezwa na ibara ya 88 ya katiba, lakini pia kwa mujibu wa taratibu zetu za kanuni. Nawashukuru mmefanya kazi nzuri na naona tuko pamoja kuendelea na shughuli zetu nyengine.

Basi Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo naomba sasa nichukue nafasi hii kumkaribisha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Karibu Mheshimiwa.

KUAKHIRISHA BARAZA

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, awali ya yote Mhe. Spika naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima uliotuwezesha kukutana katika Mkutano huu wa Tisa wa Baraza la Wawakilisi ambao unamalizika kwa mafanikio makubwa leo hii.

Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwajali wananchi wetu kuendeleza mashikamano ambao ndio nyezo kuu katika mafanikio yetu ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu. Aidha, naomba kukupongeza wewe Mhe. Spika, kwa busara zako na hekima katika kuliendesha vyema Baraza letu hili la tisa na kwa maelewano makubwa, naomba kuwapongeza pia Mhe. Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza kwa kazi wanazozifanya za kukusaidia wewe Mhe. Spika katika kuliendesha Baraza letu hili. Nachukua fursa hii pia kuwapongeza Wenyeviti na Wajumbe wote wa Kamati mbali mbali za Kudumu kwa juhudi zao kubwa wanazozichukua katika kutimiza wajibu wa majukumu yao waliopewa na kufanikisha dhamira ya Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru kiongozi wetu mpendwa Mhe. Dr. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzíbar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake thabiti uliojaa hekima, busara na upeo mkubwa unazingatia matarajio na maslahi ya taifa letu. Wananchi wa Zanzíbar wanaridhishwa kwa namna Rais wa Zanzíbar anavyoongoza nchi yetu na wamekuwa na matumaini makubwa ya kupata maendeleo katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Vile vile nampongeza sana Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad kwa jinsi anavyomsaidia Mhe. Rais katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, shukurani za kipekee nazitoa kwa viongozi wote wa serikali, vyama vya siasa na wananchi kwa ujumla kwa kuendelea kushirikiana na serikali katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzíbar yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa ni kigezo muhimu cha uzalendo, mashirikiano na umoja wetu. Serikali hii imekuwa ya mfano katika Bara la Afrika na nchi nyingi zinatupongeza kwa hatua hii muhimu tuliyofikia katika historia ya taifa letu. Sote tumeshuhudia viongozi na wageni mbali mbali wakija nchini mwetu kwa nia ya kutupongeza na kujifunza juu ya utamaduni wetu. Hivi karibuni katika Baraza hili tulipokea ugeni katika ubalozi wa Marekani nchini Tanzania na Wabunge watano wa Chama cha *ANC* kutoka Bunge la *Free State* nchini Afrika ya Kusini. Ugeni huu ulikuja kujifunza na kujionea shughuli za Baraza la Wawakilishi lenye mfumo wa kipekee duniani. Wageni wetu hao walitupongeza kwa namna tunavyoendesha shughuli zetu katika Baraza letu hili la Wawakilishi tukiwa wamoja na wenye mshikamano mkubwa.

Mhe. Spika, naomba kuwakumbusha wananchi wote juu ya umuhimu wa kuuenzi umoja na mshikamano wetu kwani hii ni hadhina kubwa kwa taifa letu na ni hidaya ya Mwenyezi Mungu kwetu kwani sote tunakumbuka nyuma tulikotoka, tutafanya kosa kubwa sana ikiwa tutaanza kuichezea amani tuliyonayo kwani kuvunjika kwa amani nchini mwetu ndio chanzo cha kuvunjika kwa umoja wetu. Hivyo basi, nawaomba wananchi na viongozi wote kuhakikisha kuwa amani, usalama na utulivu vinatawala ndani ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa dhati kabisa napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wawakilishi wa Baraza lako tukufu kwa kuwa na upeo mkubwa katika kuchangia na kushiriki ipasavyo katika kujadili miswada mbali mbali iliyowasilishwa katika mkutano huu. Kwa kweli wanastahiki pongezi kwa kujadili miswada hii kwa uwazi, ukweli na uadilifu mkubwa. Waheshimiwa Wawakilishi walitumia udhaifu wao kwa kuichambua miswada hiyo yote kwa kina na kuifanyia

marekebisho kila palipopaswa kufanya hivyo kwa nia ya kuifanya iwe bora zaidi, nawapongeza kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wawakilishi.

Mhe. Spika, napenda kwa mara nyengine kumpongeza kwa dhati ndugu yetu Mhe. Hussein Ibrahim Makungu kwa ushindi alioupata katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Bububu kwa kupitia tiketi ya Chama cha Mapinduzi, uchaguzi ambao ulifanyika tarehe 16 Septemba, 2012 kujaza nafasi iliyoachwa wazi na aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo hilo marehemu Salum Amour Mtondoo. Naitumia fursa hii kumkaribisha Mhe. Hussein na kumtakia ufanisi wa kazi zake katika Baraza hili. Aidha, natumia fursa hii kuwapongeza wananchi wote wa Jimbo la Bububu kwa kutumia haki yao ya kidemokrasia ya kumchagua kiongozi wanaemtaka na pia kudumisha amani na utulivu katika jimbo lao.

Mhe. Spika, pia nampongeza kwa dhati kabisa Mhe. Shawana Bukheti Hassan, Mwakilishi wa Jimbo la Dole kwa kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi na Waziri asiyekuwa na wizara maalum. Vile vile nampongeza Mhe. Mohamed Said Mohamed, Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Aidha, nampongeza Mhe. Mtumwa Kheir Mbarouk Mwakilishi wa Viti Maalum Wanawake kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri, Wizara ya Kilimo na Maliasili. Uteuzi wa viongozi hawa unaonesha wazi imani kubwa aliyonayo Mhe. Rais kwao kutokana na uzoefu wao na uwezo wao wa kuchapa kazi, ni matumaini yangu kwamba viongozi hawa watatumia busara na maarifa yao katika kumsaidia Mhe. Rais kuiendesha nchi yetu na kuwaletea maendeleo wananchi wetu. Ninawatakia kila la kheri na mafanikio mema katika majukumu yao mapya.

Vile vile nachukua nafasi hii Mhe. Spika, kuvishukuru vyombo vya habari vyote hasa Shirika la Habari la Zanzíbar (*ZBC*) kupitia Redio na Televisheni ambavyo vilirusha moja kwa moja shughuli za Baraza zilizokuwa zinaendelea na kuwawezesha wananchi wetu kufuatilia kwa makini hoja, michango na mijadala mbali mbali iliyoendeshwa Barazani hapa. Nazidi kuwaomba wanahabari wote wa TV, Redio na Magazeti kuitumia fursa ya kuwaelimisha wananchi juu ya mambo mbali mbali yanavyoendelea Barazani hapa kuhusu mustakabali wa nchi yao.

Aidha nachukua fursa hii kuwashukuru wakalimani wa lugha ya alama kwa kazi zao nzuri wanazoendelea kuzifanya katika kutafsiri mijadala kwa ishara ili wananchi wetu wenye ulemavu wa kutosikia nao waweze kufaidika kwa kupata taarifa mbali mbali pamoja na kufuatilia mijadala ya Baraza letu tukufu.

Mhe. Spika, Tume ya Kukusanya na Kuratibu maoni ya Mabadiliko ya Katiba hivi sasa inaendelea na kazi zake katika Mikoa ya Kaskazii Unguja na Kaskazini Bemba baada ya kumaliza kukusanya maoni ya wananchi katika mikoa ya Kusini Unguja na Kusini Pemba.

Vile vile wapo wananchi wanaoendelea kutumia fursa hii kwa kutuma maoni yao kwa tume kwa maandishi, kwa ujumla tume imeendelea kukusanya maoni kwa ufanisi mkubwa na wananchi wengi kuonekana kuitumia fursa hii kutoa maoni yao juu ya Mfumo wa Muungano wanaotaka uwepo katika nchi yao.

Kwa mara nyengine tena naomba kuwasihi wananchi wote ambao bado hawajapata nafasi ya kutoa maoni yao kufanya hivyo, kwani hii ni fursa ya pekee ya kuamua mambo muhimu yanayohusu Muungano wetu yatakayokuwa maslahi kwa wananchi na nchi yetu. Si vyema kwa baadhi ya vikundi vya wananchi kuiacha fursa hii na kuendelea kutoa matamshi yanayochochea chuki, uhasama na vurugu kwa kisingizio cha kukataa Muungano.

Jambo kubwa la kuzingatia ni kutumia fursa hii ili wananchi wote waweze kutoa maoni yao kwa uhuru bila ya kubughudhiwa. Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, taasisi za kiraia na wataalamu tujitahidi kuwaelimisha wananchi ili waepuke kulishwa maneno midomoni mwao, tuwaachie wananchi kila mmoja atoe maoni yake mwenyewe kwa mujibu wa mtazamo wake baada ya kupatiwa taaluma.

Mhe. Spika, kama tunavyoelewa wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla hivi karibuni walishiriki katika zoezi la sensa ya watu na makaazi ya mwaka 2012. Napenda kutoa taarifa kuwa zoezi la sensa ambalo lilifanyika kwa muda wa wiki mbili kuanzia usiku wa tarehe 26 Agosti, 2012 limemalizika kwa mafanikio makubwa licha ya wananchi wachache kukataa kuhesabiwa.

Napenda kuitumia fursa hii kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwashukuru wananchi wote wa Zanzibar kwa kushirikiana na serikali yao katika kufanikisha zoezi hili muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Aidha naitumia nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Taifa ya Sensa, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Wabunge, Wajumbe wa Kamati za Sensa za Mikoa na Wilaya, Masheha, wafanyakazi wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais pamoja na watendaji wote kwa mashirikiano yao yaliyowezesha kukamilisha zoezi hili muhimu katika taifa letu katika hali ya usalama na mafanikio.

Mhe. Spika, hivi karibuni nchi yetu imeshuhudia tokeo jengine muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Tokeo hili si jengine bali ni juhudi za serikali za kuwapatia nishati ya umeme ya uhakika wakaazi wa Kisiwa cha Unguja.

Kama tunavyoelewa kazi za kutandika waya mpya wa umeme wenye uwezo wa kuchukua umeme wa megawatt 100, kuanzia Ras Kiromoni hadi Fumba imezinduliwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 10 Oktoba, 2012.

Kazi hii inatarajiwa kumalizika mnamo mwezi wa Disemba, 2012 na hivyo kukifanya Kisiwa cha Unguja kuwa na uhakika wa upatikanaji wa nishati ya umeme kwa muda wote. Suala la mgao wa umeme karibuni litakuwa ni historia. Hii Mhe. Spika, ni faraja kubwa kwa wananchi wa Zanzibar kwa kuzingatia kuwa umeme ni nishati muhimu wa shughuli za uzalishaji na maendeleo ya nchi yetu. Wananchi wetu wataendelea kuitumia nishati hii kwa shughuli zao za kujiajiri kwa nia ya kujikomboa kutoka kwenye umaskini. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa kutambua mchango wa utawala bora katika taasisi za umme, sekta binafsi na taasisi za kiraia kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii, serikali inaendelea kuchukua hatua za kuimarisha taasisi za kupambana na rushwa. Hivi karibuni tu Baraza lako tukufu limepitisha Sheria Nam. 1 ya mwaka 2012 ya kupambana na rushwa na uhujumu uchumi. Hii imefuatiwa na kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi pamoja na uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo ambaye ameapishwa na Mhe. Rais hapo jana.

Naomba Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu pamoja na wananchi wote wa Zanzibar kutoa kila aina ya ushirikiano kwa taasisi hii ili iweze kutimiza majukumu na wajibu wake kwa mujibu wa sheria na kwa faida ya maendeleo ya taifa letu. Kama sote tunavyojua rushwa ni adui wa haki na hivyo haina budi kupigwa vita ili itokomezwe kabisa. Lakini juhudi hizi hazifanikiwi bila ya ushirikiano wa wananchi wenyewe.

Mhe. Spika, kuinua hali za watu wenye ulemavu ni moja ya mkakati wa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kujenga usawa na kuheshimu haki za binadamu. Naipongeza Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa juhudi kubwa wanazochukua katika kuimarisha mazingira kwa watu wenye ulemavu na kuwajengea uwezo wa kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kuwapatia watu wenye ulemavu haki zao za msingi ni jambo la Kikatiba na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itahakikisha azma hii inafikiwa.

Tunazipongeza juhudi za serikali za kuanzisha mfuko wa maendeleo ya watu wenye ulemavu. Hii ni hatua sahihi na muhimu. Hivyo viongozi na wananchi wote tunapaswa kuuchangia mfuko huu ili uweze kutimiza malengo yaliyokusudiwa katika kusogeza mbele maendeleo ya makundi yote ya watu wenye ulemavu nchini.

Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati wale wote walioanza kuuchangia mfuko huu. Vile vile namshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuongoza harambee ya kuuchangia mfuko huu uliofanyika katika Hoteli ya Zanzibar Beach Resort usiku wa tarehe 28 Septemba, 2012. (*Makofi*).

Nawaomba viongozi na wananchi wote wamuunge mkono Dr. Shein na wazidi kuhamasishana ili kila mmoja aweze kuuchangia mfuko huu. Sote tukumbuke kwamba kutoa ni moyo na wala sio utajiri. Kidogo utakachochangia italeta tofauti kubwa katika kumuendeleza mwenzetu mwenye ulemavu.

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwa masikitiko makubwa kuwa hivi karibuni katika nchi yetu tumeshuhudia vitendo vyengine vyenye kuashiria uvunjifu wa amani na utulivu na kuhatarisha umoja katika nchi yetu. Vikundi vya vijana vilijitokeza hapo tarehe 17 Oktoba, 2012 kufanya fujo na vurugu katika maeneo mbali mbali ya mji wa Unguja.

Vikundi hivyo vilichoma moto maskani kadhaa za Chama cha Mapinduzi, kuharibu miundo mbinu hasa ya barabara ambayo inaigharimu serikali pesa nyingi kuitengeneza, kuvunja maduka na kuiba mali za watu pamoja na kukatisha

shughuli za kawaida za wananchi kwa kuweka mawe na vitu vizito barabarani na kutishia amani ya wananchi. Madai ya vijana hawa ni kwamba kiongozi wao Sheikh Farid Hadi Ahmed amekamatwa na vyombo vya dola na kuwekwa ndani, madai ambayo hayajakuwa ya ukweli.

Mhe. Spika, vurugu hizi zilizoendelea kwa siku tatu ambazo zinakisiwa zilipangwa kwa makusudi zimesababisha kifo cha askari wetu asiye na hatia Koplo Said Abdulrahman, baada ya kuvamiwa na makundi ya vijana katika eneo la Bububu wakati akiwa anarejea kutoka kazini. Vespa aliyokuwa amepanda ilichomwa moto na kuteketea kabisa.

Hali hii ni ya kusikitisha sana na serikali inawasaka wale wote waliohusika na vurugu hizi na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao. Vurugu hizi ziliwafanya wananchi wenye shughuli zao za kujitafutia riski kutokana na kusimama kwa biashara zao na hasa wale wa biashara ndogo ndogo.

Tunawaomba wananchi wote Mhe. Spika, kuacha kujiingiza katika vitendo hivi vya uvunjifu wa amani, kwani kutenda hivyo ni kosa kwa mujibu wa sheria na serikali haitosita kumchukulia hatua mtu yeyote atakayejihusisha na vitendo hivi.

Aidha tunawaomba wananchi kutoa taarifa kwa vyombo vya dola mara tu wakiona dalili za watu wenye nia ya kufanya vitendo vya uvunjifu wa amani. Serikali imevumilia vya kutosha, sasa uvumilivu wake umeshafikia kikomo. Hatutomuonea haya wala kumuogopa mtu yeyote ambaye atabainika kuhusika na uvunjifu wa amani katika nchi yetu. (*Makofi*).

Aidha ninapenda kuvionya vikundi vya kihuni vinavyojiita “Ubayaubaya, Mbwamwitu, Msimbamkali na kadhalika, kuacha vitendo vyao vya kuwatisha wananchi na kuwanyang’anya vitu vyao. Huu si utamaduni wetu hata kidogo. Serikali itaendelea kuvisaka vikundi hivi. (*Makofi*).

Mhe. Spika, namuomba nichukue fursa hii kuwapa pole wale wote waliojeruhiwa au kupata madhara ya aina mbali mbali na zile familia zilizopoteza ndugu zao Mwenyezi Mungu awape subra ya kuondokewa na wapendwa wao na tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi, Amin.

Mhe. Spika, katika mkutano huu wa tisa wa Baraza lako tukufu, serikali imewasilisha miswada mitano ya sheria ambayo ina umuhimu mkubwa wa ustawi na maendeleo ya nchi yetu.

Aidha Baraza lako tukufu limepokea taarifa ya serikali kuhusu utekelezaji wa maamuzi wa Baraza yanayotokana na Kamati Teule ya Baraza ya kuchunguza mambo mbali mbali ambayo yaliibuka kwenye majadiliano ya mkutano wa bajeti wa mwaka 2011/12.

Halikadhalika Baraza lako tukufu limepokea taarifa ya Kamati Teule ya kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa. Pia Waheshimiwa Wawakilishi walishiriki katika semina mbili. Moja ilihusiana na suala la maombi ya Tanzania kutaka kuongezewa eneo la ziada la ukanda wa bahari kuu na ya pili ilihusu kupatiwa mafunzo kwa kamati ya Baraza juu ya namna ya kuwasikiliza wadau (*public hearing*).

Vile vile katika mkutano huu jumla ya maswali 62 ya msingi pamoja na maswali mengi ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wawakilishi na kujibiwa na Waheshimiwa Mawaziri husika kwa ufasaha na umakini mkubwa. Napenda kuwapongeza Mawaziri, Manaibu Mawaziri kwa umahiri wao wa kuyajibu maswali ya Waheshimiwa Wajumbe kwa usahihi kadri inavyowezekana.

Mhe. Spika, mswada wa mwanzo uliowasilishwa na kujadiliwa ni Mswada wa Sheria kuhusiana na Hifadhi na Usimamizi wa Vihatarishi vya Afya ya Jamii na Afya ya Mazingira na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Mswada huu ulikuwa na madhumuni ya kuweka sheria itakayosimamia afya ya jamii na mazingira kwa kukinga vizuri maradhi na vihatarishi vya afya ya jamii pamoja na kunyanyua kiwango cha afya cha watu ndani ya nchi yetu. Wakati wa kuujadili mswada huu, Waheshimiwa Wajumbe walionesha wasi wasi wao kuhusu utekelezaji wa sheria hii kugongana na sheria ndogo ndogo za Baraza la Manispaa. Ninapenda kuwatoa wasi wasi Waheshimiwa Wajumbe kwamba sheria mbili hizi zipo tofauti na wala hazitoathiri utendaji wa taasisi husika.

Mhe. Spika, mswada mwengine ambao uliwasilishwa katika Baraza lako tukufu ni Mswada wa Sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Madhumuni ya mswada huu ni kuanzisha wakala wa usajili wa biashara na mali Zanzibar.

Aidha sheria hii itahakikisha kwamba kazi za uwakala zinafanywa na wafanyakazi wenye sifa na ujuzi utakaowajibika kwa kuzingatia sheria, taaluma, uadilifu na maadili ya kazi. Kwa madhumuni ya utekelezaji mzuri wa sheria hii, serikali inajiandaa kuunganisha mfumo mzima wa mtandao ili kuhakikisha taarifa za makampuni zinapatikana kwa uhakika. Makampuni hayo yatapatiwa namba ya utambulisho wa mlipa kodi (Tax payer Identification Number) au Tin ili taarifa zake zikapatikane kwa usahihi katika mtandao.

Mhe. Spika, mswada wa tatu ambao uliwasilishwa ni Mswada wa Sheria ya Kuanzisha kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Mswada huu una madhumuni ya kuweka masharti ya usajili kwa taasisi za biashara na mali ili kupunguza gharama za usajili pamoja na kuondoa urasimu uliopo katika kufanya taratibu za usajili ambao umekuwa ni kikwazo kikubwa katika kuwarahisishia wananchi kusajili na kuendesha shughuli zao.

Ingawa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walikuwa wakijadili mswada huu, walionesha hofu ya kuwepo kwa mazingira ya rushwa katika utekelezaji wa sheria hii. Naomba nitumie nafasi hii kuwatoa wasi wasi Waheshimiwa Wajumbe na wananchi kwa kuwaeleza kwamba serikali imejidhatiti kupambana na rushwa mahala popote pale na kwa gharama yoyote ile, na itahakikisha kwamba inasimamia kikamilifu sheria hii ili haki ichukue nafasi yake. Sisi viongozi na wananchi wote tunahitajika kutoa ushirikiano unaostahiki ili kuifanya sheria hii itekelezeke kwa manufaa ya maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Mzanzibari Nam. 7 ya mwaka 2005 na mambo mengine yanayohusiana na hayo, nao uliwasilishwa katika Baraza lako tukufu na Waheshimiwa Wajumbe na kupata nafasi ya kuujadili kwa kina.

Marekebisho ya mswada huu una dhamira ya kuwatambua Wazanzibari wote wakaazi na wasio wakaazi wanaoishi Zanzibar. Kwa upande mwengine mswada huu una lengo la kuweka utaratibu bora wa utambuzi kwa Mzanzibari Mkaazi kwa madhumuni ya kusaidia upatikanaji wa huduma tofauti zinazotolewa na taasisi za umma. Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi ni nyenzo muhimu vya utambulisho katika maisha ya kila siku ya jamii.

Mhe. Spika, napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wananchi kwa ujumla kwamba kila mwananchi wa Zanzibar aliyetimiza masharti ya kisheria ana haki ya kupata kitambulisho. Nawasihi wale wote ambao hawana vitambulisho wafuate taratibu zilizoekwa kisheria na kuweza kupata vitambulisho vyao.

Aidha kwa wale ambao tayari wameshafuata taratibu za kujisajili na badio hawajapata vitambulisho vyao waende kwenye Afisi za Vitambulisho za Wilaya kwa ajili ya kuangalia na kuchukua vitambulisho vyao, kwani kuna vitambulisho zaidi ya 12,420 bado havijachukuliwa na wahusika.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Usajili na Usimamizi wa Maafisa wa Afya, Jamii na Mazingira na kuanzisha Baraza la Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira na Mambo Mengineyo Yanayohusiana na Hayo nao uliwasilishwa na kujadiliwa na Wajumbe wa Baraza lako.

Madhumuni ya mswada huu ni kuweka sheria itakayosimaia afya ya jamii na mazingira kwa kukinga vizuri, maradhi na vihatarishi vya afya ya jamii na wakati huo huo kunyanyua kiwango cha afya cha watu ndani ya Zanzibar.

Mhe. Spika, pamoja na miswada hiyo Baraza lako tukufu pia lilipokea miswada mengine minne ambayo ilisomwa kwa mara ya kwanza. Miswada hiyo ni:-

1. Mswada wa Marekebisho wa Sheria ya Usafiri wa Baharini Nam. 5 ya 2006
2. Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Utangazaji Zanzibar, Kazi, Majukumu na Utawala wake pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.
3. Mswada wa Sheria Kuanzisha Shirika la Meli Zanzibar, Kazi, Uwezo na mambo mengine yanayohusiana na hayo

4. Mswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa Nam. 6 ya 1997 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kama nilivyogusia hapo awali kwamba Baraza lako tukufu pia limepokea taarifa ya serikali kuhusu utekelezaji wa maamuzi wa Baraza linalotokana na taarifa ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi kuchunguza mambo mbali mbali ambayo yaliibuka kwenye majadiliano ya mkutano wa bajeti wa mwaka 2011/2012.

Kama tulivyosikia serikali tayari imeshaanza kuchukua hatua mbali mbali kwa kuzingatia sheria na taratibu za kiutawala kuhusiana na ushauri na mapendekezo ya Kamati Teule.

Vile vile Baraza lako tukufu limepokea ripoti ya Kamati Teule ya kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa. Ripoti ambayo imejadiliwa kwa hamasa kubwa. Napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba serikali imepokea taarifa hii itaitafakari, itaifanyia kazi na kuchukua hatua zipazo. Tunajua kwamba ripoti za kamati hizi zina nia ya kuisaidia serikali kuwafanya watendaji wake wabadilike na watekeleze majukumu yao kwa uadilifu.

Mhe. Spika, katika kujadili taarifa ya serikali kuhusu utekelezaji wa maamuzi ya Baraza yaliyotokana na Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi kuchunguza mambo mbali mbali yaliyoibuka kwenye majadiliano mkutano wa bajeti wa mwaka 2011/2012. Wajumbe wengi waliochangia taarifa hii walionesha kutoridhika kwao na namna serikali ilivyotekeleza maazimio hayo na kuhisi kwamba serikali inawapigia kifua au kuwalinda baadhi ya watendaji.

Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba serikali haiwezi kumlinda au kumkingia kifua mtendaji yeyote ambaye ataonekana kuhusika na utendaji wake mbovu. Nia ya serikali ni kuona watendaji wake wanatekeleza majukumu yao kwa uaminifu na uadilifu. Jambo hili tutalisimamia kwa nguvu zetu zote. (*Makofi*).

Mhe. Spika, Wajumbe wa Baraza lako tukufu wamechangia kwa busara kubwa sana na kupitisha miswada yote ya sheria ambayo imekamilisha hatua zake zote na ambayo utekelezaji wake ni muhimu sana katika ustawi na maendeleo ya nchi yetu. Serikali yetu itatilia mkazo utungaji wa kanuni kwa kila sheria ili kurahisisha utekelezaji wa sheria hizi.

Mhe. Spika, raslimali kubwa ya Wazanzibari ni amani na utulivu. Hivyo napenda kuwanasihi wananchi wote wadumishe amani, umoja na mshikamano wao na wajiepushe na vitendo vyovyote vile vinavyoashiria uvunjifu wa amani na sheria za nchi.

Ni vyema na sisi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tuendelee kuwasihi na kuwashauri wananchi wetu juu ya umuhimu wa kulinda na kudumisha amani na utulivu ndani ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kuhusu suala la mafuta na gesi asilia kutolewa kwenye mambo ya Muungano, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba viongozi wetu; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dk. Jakaya Mrisho Kikwete na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein wameafiki kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iendelee na hatua za kuanza matayarisho ya mfumo wa kisheria na kitaasisi kwa kulisimamia na kuliendesha suala hilo ndani ya Zanzibar, wakati hatua za kufanya marekebisho ya kisheria na kiutawala yanayohitajika yakiendelea kukamilishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kufuatia maafikiano hayo tayari nimeshamuandikia Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumuelezea juu ya maafikiano hayo na kupata makubaliano hayo kwa maandishi baada ya kuona kwamba maamuzi hayo hayapinzani na Katiba wala sheria. Si baada ya muda mrefu suala hili litakamilika na kuliarifu Baraza lako tukufu kwa ukamilifu katika kikao kijacho.

Kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hatua tunazozihitaji kuzichukua kwa haraka ni pamoja na kukamilisha mfumo wa kiutawala na utekelezaji wa sera ya nishati ya Zanzibari, kuandaa mswada wa mswada ya usimamizi na uzalishaji wa mafuta na sheria ya kuanzisha rasmi chombo cha kusimamia suala la utafutaji na uzalishaji mafuta Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa hekma na busara zako binafsi zilizopelekea kuliongoza Baraza hili kwa mafanikio makubwa.

Aidha napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa uvumilivu waliouonesha kwa muda wote wa mkutano wa Baraza hili, pia kwa umakini waliouonesha katika kuyajadili na kuyapitisha mambo mbali mbali yaliyoletwa mbele yao.

Nawashukuru sana, nawatakia safari njema ya kurejea kwenye majimbo yao kwa ajili ya kuwatumia wananchi wao. Kwa vile hatutoonana tena kabla ya sikukuu ya Idd EL Hajj, nachukua fursa hii kukutakieni Idd Hajj njema na Eid Mubaraka.

Pia Mhe. Spika, nakutakia mwaka mpya 2013 wa baraka na mafanikio mema.

Mhe. Spika, mwisho kabisa napenda kuwashukuru sana watendaji wako wote wa Baraza la Wawakilishi kwa juhudi walizochukua katika kufanikisha kazi za Baraza hili tukufu. (*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kutoa hoja ya kuliakhirisha Baraza lako tukufu hadi siku ya Jumatano tarehe 16 Januari, 2013.

Naomba kutoa hoja. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa hotuba ambayo inatufungia shughuli zetu za mkutano wa tisa. Amegusa mambo yote ya Baraza hili ambayo tumeyafanya lakini pia amegusa mambo na matokeo mbali mbali yaliyotokea nchini mwetu.

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais tunakushukuru sana kwa hotuba hii nzuri.

Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa basi niwahoji wale wanaokubaliana kuakhirisha mkutano wetu huu wa Tisa hadi tarehe 16 Januari, 2013 saa 3. 00 asubuhi wanyanyue mikono. Wanaokataa, Mhe. Saleh yeye anasema tuendelee tu.

Nawashukuru , waliokubali wameshinda.

Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaakhirisha mkutano huu kuna matangazo matatu.

Tangazo la kwanza tuliona kwamba tuitishe Kamati ya Uongozi ili tupate mawazo kuhusiana na masuala ya Tume yetu ya Utumishi ya Baraza lakini na Tume ya Utumishi Serikalini.

Sasa Kamati hiyo ya Uongozi ya Baraza tunategemea tukutane pale ukumbi wa juu mara baada ya kuakhirisha mkutano huu. Nafikiri tayari tumealikwa Wajumbe wa Kamati ya Uongozi wa Baraza na mara baada ya kumaliza shughuli hii tukutane pale ili tuelezane baadhi ya mambo. Hautokuwa mkutano mrefu utamaliza muda usiokuwa mkubwa.

Lakini pili kutakuwa na semina iliyoandaliwa na Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Semina hii itakuwa kesho hapo hapo kwenye ukumbi wa juu. Semina itaanza saa tatu kamili za asubuhi. Wajumbe usajili utafanyika saa mbili na nusu asubuhi ili tuweze kufanya semina hiyo saa tatu barabara za asubuhi.
Semina hii nayo haitokuwa ndefu, kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe tusiwe na hofu mara baada ya semina hiyo itakuwa tuna nafasi sasa ya kurudi majumbani mwetu kwa ajili ya kusherehekea Idd El Hajj.

Tangazo la tatu ni tangazo la Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwamba Waheshimiwa Wajumbe wanawake ile mazoezi yao yatafanyika katika viwanda vyetu vya Baraza tarehe 15 mwezi wa kumi na moja hapa hapa mapema kabisa asubuhi kwenye viwanja vya Baraza.

Wawakilishi wanawake munaombwa muhudhirie kwenye mazoezi ili kulinda afya.

Lakini mwisho kabisa nichukue nafasi hii Waheshimiwa Wajumbe kuwashukuru sana kwa mashirikiano makubwa na mimi nitoe mkono wa Idd kwenu, kwa sababu hatutokutana mpaka baada ya Idd na kwa kweli baada ya mwaka

mpya ujao. Kwa hivyo nitoe mkono wa Idd El Hajj kwa Wajumbe wote mukasherehekee vizuri kama mheshimiwa alivyosema, lakini pili vile vile tunawatakia mwaka mpya mwema.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe, sasa ninaakhirisha mkutano huu wa tisa hadi tarehe 16 Januari, 2013 saa tatu barabara za asubuhi.

(WIMBO WA TAIFA)

(Saa 4.30 asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 16/01/2013 saa 3.00 asubuhi)